

## **LBE KOMPUTA NA INTANETI - Programme 5**

(Only Part 5.1 as central script, part 5.2 about products and websites in African Languages is supposed to be done by each language department)

Mwandishi: Richard Lough

Muhariri: Maja Dreyer

Tfasiri: Eric Ponda

**Wahusika:** John (Mvulana wa Makamu), Mtaalam ( Sauti kutoka Studio)

**Sauti:** Daniel Gichuki (Mwalimu wa umri wa makamu ), Mark Sewe  
(Mvulana katika Mkahawa wa Intaneti.)

**Sauti Nyingine** ya pili kutoka Studio.

### **Muziki**

#### **Intro**

Hujambao na karibu katika kipindi kingine kuhusu komputa na Intaneti.. Katika kipindi hiki cha tano, John anajifunza jinsi Mtandao wa Intaneti ulivyo chombo muhimu katika shughuli za utafiti. Matumizi ya mtandao wa Intaneti kwa kweli hayana mwisho. Mradi tu uwe unaweza kuutumia vyema na kujua unachotafuta katika mtandao. Nataraji utaandamana nasi hadi mwisho wa kipindi wakati John anapozungumza na Mkufunzi wa chuo cha mafunzo ya Teknolojia ya Mawasiliano jijini Nairobi nchini Kenya. Pia utasikia ushauri na mawaidha kutoka kwa mtaalam wetu wa Intaneti hapa studioni.

#### **5.1\_SFX\_Kituo cha mafunzo IAT\_e**

**1. John** I Sasa niko katika chuo cha mafunzo juu ya Teknolojia ya mawasiliano jijini Nairobi. Niko naye Mwalimu wangu Daniel Gichuki [gi-CHU-ki]. Sasa Daniel nimesikia neno linalotumika wakati Mtu anapotumia huduma hizi za mtandao wa Intaneti kufanya utafiti. Neno lenyewe ni “*Search Engine*” yaani Injini ya Utafiti. Neno hili linamaanisha nini hasa?

### **Clip: 5.1\_Gichuki\_1**

Neno *search engine* ni programu unayoweza kutumia katika mtandao wa Intaneti kutafuta habari unazoitaka kutoka kwa mtandao au ukurasa fulani. Chochote kile unachotafuta kwenye mtandao.

**2. John** Programu hii hufanya kazi vipi?

### **Clip: 5.1\_Gichuki\_2**

Unachopasa kufanya ni kuandika neno unalotaka kwenye ukusara wa *Search Engine* na kisha programu hii itatafuta habari unazotala kutoka kwa mtandao..

**SFX: Beep sound (should always be used to introduce the expert, like somebody answering in a quiz show)**

**3. Mtalaam** Hebu sasa nikufafafanulie zaidi kuhusu maelezo ya Daniel. Huduma hizi za utafiti hutumia programu

maalum ijulikanayo *Spider* yaani Bui bui.

Huchunguza yenyewe mtandao wa Intaneti na kuweka hifadhi au *Database* habari zote unazotafuta.

*Spider* au bui bui kama tulivyowaita hapo mbeleni hukusanya na kukagua habari zote zilizoko kwenye ukurasa wa mtandao. Kisha habari hizi hutumwa kwa kitengo maalum cha ukurasa wa utafiti au *search Engine*. Kwa hivyo wakati unapotafuta habari kupitia kwa programu hii ya utafiti, maneno uliyoandika kwenye ukurasa hutafutwa kwenye orodha ya hifadhi ya kurasa zote kwenye mtandao. Na kisha kukutolea habari zinazohusiana na maneno unayotafiti..

**4. John:** Ahha ! ni vigumu kuelewa! Daniel, kuna programu nyingine bora zaidi na ya uhakika mtu anaweza kutumia?

### Clip: 5.1\_Gichuki\_3

Watu wengi hupenda na kuamini sana ukurasa wa tovuti ya *Google* ambao ni madhubuti na wa kuaminika katika shughuli hizi za utafiti, lakini pia kunazo kurasa za tovuti nyingine kama vile *Yahoo*, *MSN* na kadhalika..

**5. John:** Sasa umewadia wakati wa kuzungumza na Mark Sewe mwenye umri wa miaka 19 ambaye yuko darasa jingine karibu kidogo na darasa letu. Mark

alimaliza masomo yake ya shule ya sekondari mwaka uliopita na sasa anasababu zote za kutumia mtandao wa Intaneti.... Yeye anataka kwenda kusomea ng'ambo.

### **X-fade from 5.1\_SFX\_IAT\_Centre into 5.2\_SFX\_Sewe\_Classroom**

#### **Clip\_5.1\_Sewe\_1**

Natafuta chuo kikuu ambacho ni cha gharama nafuu na kinachotoa mafunzo mazuri ili niweze kujifunza taaluma nizitakazo. Hapa nimeona vyuo vingi tu mpaka nimechanganyikiwa....

#### **6. John:**

Lakini Mark, utajuaje habari unazozipata kwenye mtandao kuhusu vyuo hivi ni za kuaminika?  
Unauhakika gain kwamba habari hizi ni sahihi.?

#### **Clip: 5.1\_Sewe\_3**

Kwanza kabisa kuna kurasa nyingi unazoweza kutafuta habari hizi, kwa hiyo chaguo ni lako.

Ukitafuta habari hizi kutoka kwa kurasa tofauti na ziwe zinazofafana, basi kumbuka kwamba zina ukweli fulani. Na pia unapasa kuelewa si rahisi Mtu kutuma habari za uongo kwa mtandao wa Intaneti. Sijui kwa maoni yako lakini mimi ninaamini sana habari ninazopata kwenye mtandao wa Intaneti

**SFX: Beep sound**

**7. Mtalaam:** Wooaahh! Hebu ngoja kwanza . Samahani huwezi kuamini kila kitu unachokiona kwenye mtandao wa Intaneti. Kila mtu yuko huru kutuma habari zake kwenye mtandao . Na zaidi kuna kurasa nyingine kama vile *encyclopaedia, Wikipedia*, ambazo ziko wazi kutumiwa na kila mtu yaani “*open source*”.

**8. John:** Nini maana ya “*open source*”?

**9. Expert:** Hii inamaanisha mtandao wazi, yaani Mtu yoyote yuko huru kutuma habari zake kwa ukurasa wa mtandao wa Intaneti. Lakini kumbuka unapasa kuelewa kwamba ukurasa wa *Wikipedia* ni ukurasa unaoaminika. Lakini Ni lazima uhakikishe utafiti wako na kurasa nyingine ili kubaini uhakiki wa habari hizo.

**10. John:** Asante sana kwa ufafanuzi wako , sasa umeonywa Mark!

*LBE Komputa na Intaneti - Programme 5.2*

**Wahusika:** Beatrice (Msichana wa makamu), John ( Mvulana wa makamu), Komputa (sauti ya Mwanamke), Msaidizi ( Sauti ya Mwanamke)  
**Sauti ya Msimulizi: kutoka Studioni.( Kurekudiwa Bonn)**

**Music – [Full up for 0.10 then fade]**

SFX\_Mtandao ukifunguka [Sauti ikitoweka chini kwa chini.]

- 1. Komputa:** Habari John na Beatrice....
- 2. Beatrice:** Habari Komputa . Au niseme Jambo, habari.
- 3. Komputa:** Ahha Beatrice, ...kwa hivyo unataka tuzungumze kwa lugha yako ya Kiswahili.?
- 4. Beatrice:** Ndio ikiwezekana. Kwa kweli Komputa, nimekuwa nikifanya kazi zangu za Shule kwa lugha ya Kingereza na hutumia lugha hii ninapokuwa kwenye mtandao. Lakini lugha yangu ya kwanza ni Kiswahili.. Ndio lugha ninayozungumza nyumbani nikiwa na marafiki na Familia yangu.Ningependa kujua iwapo kuna kurasa za tovuti kwa lugha hii ya Kiswahili kwenye mtandao.
- 5. Komputa** Hebu subiri kidogo nijiunganishe na Mtandao. Lakini nadhani kuna kitengo cha usaidizi yaani “*Help*” katika mtandao hebu tuulize.

**6. Beatrice:** Asante sana Komputa.

**7. Komputa:** Sawa sasa tumeunganishwa. *“Help”!* upo?

**FX Sauti ya \_Help\_ikiunganisha mtandano.**

**8. Help:** Habari Komputa. Naweza kuwasikia hapo ukiwa na rafiki zako John na Beatrice.

**9. John:** Tulikuwa tunauliza Komputa iwapo kuna kurasa za tovuti kwa lugha yetu ya Kiswahili au lugha nyingine za Kia-Africa.?

**10. Help:** Ndio zipo. Lakini sio nyingi vile, hasa ikizingatiwa kwamba lugha ya Kiswahili inazungumza sana katika eneo la Africa Mashariki.

**11. John:** Kweli? Ukisema hivyo unamaanisha nini., Help?

**12. Help:** Labda ni kwasababu kuna lugha nyingi Barani Africa. Kwa hivyo si dhani kama Mtandao umefanikiwa kunasa lugha hizi zote . Lakini baadhi ya vyombo vya habari hutoa habari kwa lugha zao. Kwa mfano tunaweza kuanza na mtandao wa idhaa ya Kiswahili ya Radio Deutsche Welle. Pia shirika la utangazaji la BBC linamtandao wake.

**SFX\_Akiandika / Sauti za vipindi vya Kiswahili kutoka mtandao wa DW?**

**13. Beatrice:** ...www.dw-world.de/kiswahili... - www dot dw dash world dot de slash Kiswahili. Sivyo?! Sawa, umefunguka sasa. Ahha, unatoa habari kem kem kwa lugha ya Kiswahili. Na pia nikiendelea chini kidogo kuna idhaa nyingine katika lugha mbali mbali zinazotupa habari. Kuna idhaa ya Kiarabu, Ki-Hausa, Kireno na kadhalika.. ziko nyingi!

**14. Help:** Ndio , mtandao wa Intaneti ni muhimu sana hasa kwa watu wanaotaka kusoma au kusikiza habari kwa lugha zao badala ya Kingereza..

**15. John:** Beatrice, unakumba yule rafiki yako kutoka Sudan muliyekuwa mukiwasiliana kupitia mtandao? Lazima awe anazungumza Kiarabu. Sina hakika kama kunatovuti katika lugha ya Watu wa Sudan.

**16. Help:** Ndio ziko kurasa nyingi kwa lugha ya Kiarabu, kwani huzungumzwa na wengi ndani na nje ya Africa. Na ukifungua ukurasa wa Jumuiya ya Africa, utakuta lugha ya kiarabu inatumiwa zaidi kama lugha rasmi katika ukurasa wa tovuti hiyo..



**17. John:** Ukurasa wenyewe ni [www.africa-union.org](http://www.africa-union.org) - *www dot Africa dash union dot org*. Hebu kidogo ufungue. Ah ndio, Naona maandishi kwa lugha ya Kirabu . Na nikiufungua zaidi, lugha inayotumika ni Kiarabu ingawa sielewi lugha hii..

**18. Help:** Kuna kurasa nyingi munaweza kuendelea kutafuta kurasa hizi kwa kupitia Search engines hasa katika ukurasa wa Google. Namtakia kila la kheri . Najua mutakuwa na shughuli nyingi.

**19. J&B:** Asanhte sana kwa usaidizi wako, umetupa changamoto ya kuendelea kutafakari. Kwaheri !

## **Outro**

Ni hayo tu tuliyoweza kukuletea katika kipindi hiki. Kumbuka kuna kurasa nyingi katika lugha ya Kingereza na nyingine mbali mbali za Kiafrika zilizo na habari muhimu . Ukitaka kujifunza mengi zaidi kuhusu Komputa au kusoma kupitia mtandao wa Intaneti ungana nasi kwa kipindi kijacho cha Learning By Ear. Pia ukiwa unataka kukisikiliza tena kipindi hiki pamoja na marafiki zako, tembelea tovuti yetu: [www.dw-world.de/lbe](http://www.dw-world.de/lbe) Hadi wakati mwengine kwaheri.